



*Taarifa kwa Vyombo vya Habari
September, 2013*

Watumishi wanaofanya mapenzi na wagonjwa waadabishwe!

Tunasikitishwa na tunalaani mwendelezo wa ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma unaofanywa na baadhi ya watumishi wa afya. Hivi karibuni imeripotiwa na vyombo vya habari kwamba watumishi wawili wa afya katika zahanati ya Mwanhala wilayani Nzega wanatuhumiwa kuwataka kimapenzi wagonjwa. Taarifa hizo pia zilieleza kwamba mmoja wa watumishi hao amewahi kukutwa akifanya 'mapenzi' wodini na mgonjwa, nyakati za kazi.

Taarifa nyingine za ukiukwaji wa maadili ziliripotiwa kutokea katika hospitali ya Mbagala Zakheim ambapo muuguzi alidaiwa kukataa kumhudumia mama mjamzito aliyeshikwa na uchungu kwa kumwambia aje siku inayofuata.

Kwa mtazamo wetu, mifano hiyo ya ukiukwaji mkubwa wa maadili ya kazi kwa watumishi wa afya si tu kwamba unadhaliisha taaluma hiyo muhimu bali pia unaathiri wananchi wanaotumia huduma za afya. Mwenendo huo pia unatishia haki ya wananchi ya kupata huduma bora za afya kwani wengi wanaweza kuwa na hofu hivyo kusita kutumia huduma hizo na kuathirika zaidi kiasya.

Ili kurekebisha ukiukwaji wa maadili ya watumishi wa afya, Sikika inatoa wito kwa kamati za maadili za halmashauri na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma- Kitengo cha Maadili, kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wote wa umma wanaokiuka maadili ya kazi badala ya kuwahamishia kwenye vituo vingine.

Sikika inampongeza Mkuu wa Wilaya (DC) ya Nzega, Bi. Tunu Msangi kwa kukemea vitendo vya ukiukwaji wa maadili ya watumishi wa afya wilayani Nzega na kutoa wito wa kuchukuliwa kwa hatua kali za kisheria dhidi yao. Alipozungumza na Sikika kwa njia ya simu, mkuu huyo wa wilaya alisema '*...kwa sasa uchunguzi wa kina juu ya suala hilo la watumishi kufanya mapenzi na wagonjwa unaendelea na iwapo watathibitika kutenda kosa hilo lazima watachukuliwa hatua za kisheria, hatuwezi kuendelea kuvumilia mambo kama haya*'. DC Msangi pia alipinga utaratibu wa kuwahamisha watumishi hao kama ilivyokuwa imepangwa na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo.

Sikika inatoa pongezi pia kwa wananchi wa Kata ya Utwigu (Nzega) kwa kuchukua hatua na kupeleka malalamiko kwa diwani wao ambaye naye aliwajibika na kuwasilisha malalamiko hayo katika Baraza la Madiwani wa halmashauri ya Nzega.

Mfano huo wa wilayani Nzega unathibitisha kwamba iwapo kila mtu atawajibika kwa nafasi yake, huduma zinazotolewa na taasisi za umma zikiwemo za afya zitaboreka.

Mr. Irenei Kiria, Mkurugenzi Mtendaji

P.O.Box 12183 Dar es Salaam,

Tel: +255 222 666355/57, Cell: 0784 274039, Fax: 2668015,

Email: info@sikika.or.tz,

Twitter: @sikika1, Facebook: Sikika Tanzania, Website: www.sikika.or.tz